# 16 JE, KUNA MAISHA BAADA YA KIFO?




Mara nyingi, tunashangaa kwamba kunatokea nini baada ya kifo. Kuna wale ambao, baada ya tukio wamehuishwa na kueleza juu ya mambo waliyoyafahamu kwenye kifo. Mara nyingi tunasikia ya kwamba waliokufa wamejidhihirisha wenyewe; wengine hata kuongea nao.

Je, inafaa kuogopa kifo?

Mara kwa mara tumekutana na kifo ana kwa ana; tunapohudhuria mazishi ya rafiki ama ndugu kwenye kumuaga, ama pale tunapoliona lile gari la kuchukua maiti mazikoni likifuatiwa na waombolezaji waliovalia mavazi meusi. Tunashangaa, kuna maisha baada ya kifo? Pengine pale tunapoweka mashada ya mauwa juu kaburi tunajiuliza wenyewe, je, wafu wanao ufahamu wo wote?

Mke, akiwa amevunjika moyo kutokana na uchungu na kububujikwa na machozi, anashangaa, hivi nitakuja kumwona tena?

Kuna maoni mbalimbali juu ya jambo hili. Wengine wanasema ya kwamba mtu anapokufa huenda moja kwa moja mbinguni, purgatori ama kuzimu; wengine wanaamini ya kwamba amekwenda kwenye ulimwengu wa roho ama anafanyika upya na kuzaliwa kuwa kiumbe kipya; wengine bado wanasema ya kwamba hapa yote yamefikia mwisho wake; wengine wanasema ya kwamba mtu aliyekufa hafahamu kitu cho chote hadi siku ile ya ufufuo. Ni nani aliye sahihi? Kwani Mungu amesemaje? Biblia inatupatia jibu gani? Ayubu 14:14.

## MCHAKATO WA UHAI NA KIFO

**1. Ili kuufahamu mchakato wa kifo, kwanza na tutafakari kama ni jinsi gani uhai ulivyoanza? Mwanzo 2:7.**

______________________________________________________________

*Mwanadamu amefanyizwa kwa vitu viwili. Mungu alichukua kitu cha kwanza kutoka katika mavumbi ya ardhi. Mwili wa mwanadamu umefanyizwa kwa protini, mafuta, madini (kama vile fosforasi, chuma, magnesia, kalshamu, n.k.), na asilimia kubwa ni maji. Kiasi cha thamani halisi ya vitu hivi si zaidi kuliko $5; hii ndio thamani ya vitu vya mwili wetu. Tungekuwa na thamani ndogo kiasi gani kama isingekuwa ni pumzi ya uhai ya Mungu! Muunganiko wa vitu hivi viwili ndivyo vilivyomfanya mwanadamu, kiumbe kipya kabisa.*

a) Kama tungelifafanua jambo hili kwa mlinganisho wa kihisabati tungesema:
**kitu (udongo) + pumzi ya uhai = nafsi hai** (nafsi inayoishi).

b) Pale Mungu alipomwumba mwanadamu, mwanadamu akawa nafsi hai; haisemi ya kwamba Mungu alitoa nafsi ama kwamba mwanadamu anayo nafsi, bali munganiko wa mavumbi ya udongo na pumzi ya uhai ukamfanya yeye kuwa nafsi hai; kwa hiyo, mwanadamu ni nafsi. Pale tunaposema ya kwamba nafsi 3,000 walibatizwa, hatusemi kwamba roho 3,000 zilibatizwa bali ni watu.

c) Kuna mazao tofauti ya kikemikali ambayo, yanapochanganywa, huleta kitu kingine tofauti kabisa. Kwa mfano, ukichanganya atomi mbili za haidrojini pamoja na moja ya oksijini, tunapata maji, H20.

d) Iwapo taa ya umeme inapokea umeme, inatoa mwanga kutokana na mkondo wa umeme ulioifikia. Pale nishati hiyo inapozuiwa, ile nuru hutoweka. Ile taa haiwezi kutoa nuru yenyewe, wala umeme wenyewe hautoi nuru wenyewe.

**2. Maadamu mchakato wa kifo ni kinyume cha uhai, je, ni nini hutokea pale mtu anapokufa? Muhubiri 12:7; Zaburi 104:29.**

______________________________________________________________

***Kitu (udongo) – pumzi ya uhai = kifo.*** *Kama ilivyo katika jambo la taa, udongo unakuwa hauwezi cho chote pale Mungu anapoondoa ile pumzi ya uhai.*

## *JE, KIFO NI KUWA KATIKA HALI YA UFAHAMU?*

**3. Je, wafu wanafahamu kitu cho chote? Mhubiri 9:5.**

______________________________________________________________________

**4. Kunatokea nini juu ya hisia zao? Mhubiri 9:6, 10.**

______________________________________________________________________

**5. Je, wafu wako katika hali ya ufahamu wo wote? Zaburi 146:4.**

______________________________________________________________________

**6. Je, wafu wanajua lo lote juu ya jamaa zao? Ayubu 14:21.**

______________________________________________________________________

**7. Je, wako mbinguni wakimsifu Mungu? Zaburi 115:17; Isaya 38:18, 19.**

______________________________________________________________________

## *KIFO KINAFANANISHWA NA NINI?*

**8. Je, Yesu anakifananisha kifo na nini? Yohana 11:11 -14.**

______________________________________________________________________

*Ayubu naye anakifananisha kifo na usingizi. Wafu wamelala; hawana ufahamu wo wote hadi pale watakapoamka katika ule ufufuo. Ayubu 14:10-12.*

**9. Je, ni mfano gani mwingine ambao Maandiko hutupatia? Ayubu 14:1, 2.**

______________________________________________________________________

## *JE, TUTAWAONA TENA WALE WALIOKUFA?*

**10. Je, tumaini lenye utukufu la wale walikufa wakimwamini Mungu ni lipi? Isaya 26:19; 1 Wathesalonike 4:14-17.**

______________________________________________________________________

**11. Je, wale waaminifu wa kale waliokufa tayari wanafurahia uzima wa milele? Waebrania 11:39, 40; Danieli 12:13.**

______________________________________________________________________

*Kuna mkanganyiko kati ya wale wanaohubiri ya kwamba kuadhibiwa ama kuzawadiwa hufanyika mara moja, na wakati huo huo wanahubiri juu ya ufufuo na ile hukumu. Iwapo mtu anapoikea tuzo yake pale anapokufa, ni kwa nini basi Yesu aje kuwahukumu wafu na walio hai? Atahukumu nini? Je, ni kipi kilichopokelewa tayari?*

## *UDANGANYIFU MKUBWA, NA MKONGWE ZAIDI ULIOWADANGANYA MAMILIONI*

**12. Mungu aliwaambia Adamu na Hawa ya kwamba kama wangekosa kutii wangekufa (Mwanzo 2:16, 17). Hata hivyo, uongo mkubwa wa Shetani ulikuwa ni nini? Mwanzo 3:4.**

______________________________________________________________________

*Kwa miaka 6,000, Shetani amehubiri uongo huu, ambao umeaminiwa na karibu ya waungwana wengi. Desturi za ibada za wafu zilikuwapo miongoni mwa Wamisri, ambao waliweka samani, vyakula, hazina za thamani ndani ya makaburi ya Mafarao. Kuna mamilioni hivi leo ambao huamini ya kwamba wale wafu wanafurahia uzima wa milele ama wanateseka na adhabu kule kuzimu ama purgatori.*

**13. Je, ni nani pekee asiyefikwa na umauti? 1 Timotheo 6:15, 16.**

____________________________________________________________

*Yesu anataka kuwapatia hali ya kutofikwa na umauti watoto Wake, pale ajapo mara ya pili. 1 Wakorintho 15:51-55.*

**14. Je, tunayo tayari hali ya kutokufa, ama tunaitafuta? Warumi 2:7.**

____________________________________________________________

## *HITIMISHO*

Kifo ni kinyume cha uzima. Pale mtu afapo, anakoma kuwapo; anakuwa hana ufahamu. Licha ya hili, tumaini letu kubwa liko katika kuja kwa mara pili kwa Yesu, pale tutakapokutana na wapendwa wetu waliokufa katika Kristo.

**15. Hatimaye Yesu atafanya nini na kifo? Ufunuo 21:4.**

____________________________________________________________

Daima tunapasa kujitayarisha kwa sababu maisha yetu yananing’inia kama kwa uzi.

***Uamuzi wangu:*** *Ninaamini ya kwamba wafu hawajui kitu cho chote, nao wanalala hata ule ufufuo wa mwisho.* ○ *Ndio* ○ *Hapana*